

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA THELATHINI NA TANO**

**01 JUNI, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA TANO – TAREHE 01 JUNI, 2022

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NISHATI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 305. MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la kubeba Wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mkalama.



#### 306. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Mundindi, Lupingu, Lupanga, Ludende, Madilu, Ludewa, Lugarawa na Mawengi utakamilika.

**307. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO  
(MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha kwa barabara Kata za Ulaya, Kisanga, Malolo na Uleling'ombe katika Jimbo la Mikumi.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**308. MHESHIMIWA ESTER EDWIN MALEKO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango):-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kutoa msamaha wa kodi ya jengo kwa wanaostahili baada ya kodi kuhamishiwa kwenye LUKU.



## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **309. MHESHIMIWA KILUMBE SHABAN NG'ENDA (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kuna mpango gani wa kukiendeleza Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ili kiwe Chuo kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **310. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali imetekeleza kwa kiwango gani Mkakati wa Afrika wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STISA – 2024).

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**311. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA  
KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,  
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu ya  
mawasiliano katika Kata za Idete, Kiyowela,  
• Maduma, Idunda, Makungu na Ihowanza. •

**WIZARA YA MAJI:**

**312. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA KITANDULA  
(MKINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Wananchi wa Kata ya Bosha na  
Mhinduro watapata maji salama.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**313. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA  
KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha Maporomoko ya Kalambo yanatangazwa ili yawe na mchango wa kiuchumi kwa Taifa.

**314. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI  
MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti Tembo wanaoharibu mazao na kujeruhi Wananchi Kata za Mindu, Kahulu na Tinginya - Tunduru.

**WIZARA YA AFYA:**

**315. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY  
(MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha kuwa Vyumba vya kuhifadhi maiti nchini vinakuwa na majokofu.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA NISHATI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA**  
**01 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**